

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR
MTIHANI WA KURINGILIA KIDATO CHA TATU

202

KISWAHILI

MUDA: SAA 2:30

JUMATATU 4 DISEMBA, 2023 MCHANA

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C, na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
JUMLA		
SAINI YA MHAIKIKI		



Mtihani huu una kurasa 14 zenye maandishi

SEHEMU A: (Alama 20)

UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Soma kwa makini habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Katika miaka ya hivi karibuni yasemekana kuwa, Tanzania imekumbwa na wimbi kubwa la vitendo mbali mbali vinavyohusishwa na imani za kishirikina katika pembe zote za nchi yetu. Sio kwamba imani za kishirikina zimeanza siku hizi, isipokuwa zamani hazikuwa zikiambatana na uhalifu wa kiwango kikubwa na cha kutisha kama ilivyo hivi sasa. Vitendo hivyo ni pamoja na mauaji ya vikongwe ambayo yanasikika zaidi katika mikoa ya kanda ya ziwa kama vile Shinyanga na Mwanza. Vikongwe wengi wasio na hatia wameuwawa kikatili kutokana na tuhuma za uchawi. Vikongwe hao wanadaiwa kuwaua ndugu na jamaa zao ambao nao huamua kuwaua kutokana na tuhuma hizo.

Hivyo, ni suala la kujiuliza, mtu anawezaje kushughulikia uhalifu kwa kutenda uhalifu? Anawezaje kutibu tatizo la uuaji kwa kumuua muuaji? Watu wengi wanaelezea kuwa, matendo hayo hutendeka pale watu wanapoondokewa na wapendwa wao wa familia, hivyo huenda kwa wapiga ramli ili kubaini kilichowaua ndugu zao. Hapo ndipo baadhi ya waganga wa kienyeji huwaambia wateja wao kwamba ndugu zao wameuliwa na bibi au babu fulani. Kitendo hicho huamsha hasira kwa watu hao na kuamua kwenda kuwaua kikatili watuhumiwa wakiwa wanaamini kuwa kufanya hivyo ndio kusuluhisha tatizo au kulipiza kisasi.

Pia, mnamo miaka iliyopita iliripotiwa kuwepo kwa mauwaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi yaani albino. Watu hao makatili huwachuna ngozi zao au kukata sehemu za miili yao. Unyama huo ulisababisha watu wengi wasio na hatia kupoteza maisha. Watu wengi waliuliwa na ngozi zao kuuziwa waganga wa kienyeji.

Tatizo hilo linawiyana na yale yanayotokea kanda ya ziwa. Katika eneo hilo washirikina wenye roho za kinyama huwaua watu wenye ulemavu wa ngozi kwa kuvamia nyumba zao nyakati za usiku na kuwakata viungo. Hali hii huwaacha walemavu hao na maumivu makali pamoja na ulemavu mwingine wa viungo.

Wakati sasa umefika kwa serikali, wananchi na vyombo vya habari kushirikiana ili kupiga vita unyama huo usikubalike hata kidogo katika jamii. Hii ni pamoja na kuwachukulia hatua waganga na wateja wanaojishughulisha na vitendo hivyo viovu.

MASWALI

- a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kutokana na habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi matano (5).

- b) Mauaji ya vikongwe yanafanyika zaidi maeneo gani nchini Tanzania?

- c) Taja sababu inayopelekea vikongwe wengi kuuwawa kikatili.

- d) Eleza kwa ufupi namna waganga wa kienyeji wanavyochangia mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

- e) Mwandishi anashauri jambo gani lifanyike ili kuzuia mauaji ya kikatili?

2. Fupisha aya ya mwanzo ya habari uliyoisoma hapo juu kwa maneno yasiyozidi ishirini (20).

SEHEMU B: (Alama 30)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii. Swali la TANO (5) ni la lazima.

3. a) Kwa kutumia mifano eleza kazi tatu (3) za viambishi awali.

- b) Tumia mzizi –lim– kuunyumbulisha katika kauli na hali zifuatazo.

- i. Urejeshi

- ii. Ukanushi nafsi ya tatu umoja

- iii. Kauli ya kutendea

- c) Kwa kutumia mifano fafaua kazi zifuatazo za mofimu “ki”.

- i. Kutambulisha udogoshi

- ii. Kutambulisha ushuruti

d) Kwa kutumia njia ya uambishaji wa maneno, nominisha vitenzi vifuatavyo.

i. Nenda

ii. Piga

e) Vipange vielezi vifuatavyo katika aina zake.

vibaya, alfajiri, kiasi kikubwa, humu, mara chache, mwaka juzi

4. a) Taja aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo.

i. Wanafunzi waliofika mapema ni mahodari.

ii. Kaa hatafuni kwa mdomo.

iii. Ama kweli! Dunia hadaa, ulimwengu ni shujaa.

b) Tunga sentensi mbili (2) ukitumia viambishi vioneshi kisha eleza umbali au ukaribu wake na mzungumzaji.

i. _____

ii. _____

- c) Tafautisha kati ya viwakilishi vya pekee na vivumishi vya pekee.

- d) Kwa kutumia mifano eleza aina mbili (2) za vitenzi vishirikishi vikamilifu.

i. _____

ii. _____

- e) Kwa kutumia mifano tafautisha kati ya vihusishi na vihisishi.

5. a) Andika mifano ya sentensi zenye makosa yafuatayo.

i. Kosa la kisarufi

ii. Kosa la kimantiki

b) Toa maana mbili (2) kwa kila tungo zifuatazo.

i. Andika neno vizuri.

ii. Ali kanipigia mpira.

c) Toa mfano mmoja (1) wa mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira yafuatayo.

i. Shuleni

ii. Mahakamani

d) Toa maana za misimu ifuatayo.

i. Teja

ii. Utajiju

iii. Buku jero

- e) Eleza sifa mbili (2) za lugha ya maandishi.

i. _____

ii. _____

SEHEMU C: (Alama 30)

FASIHI

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii. Swali la SITA (6) ni la lazima.

6. a) Nini maana ya usimulizi?

- b) Simulia tukio usilolisahau katika maisha yako kwa kutumia muundo wa hadithi kwa maneno yasiyozidi 120.

d) Eleza sifa mbili (2) za vitendawili.

i. _____

ii. _____

e) Toa faida mbili (2) za kazi za fasihi simulizi katika jamii.

i. _____

ii. _____

8. a) Taja vipengele vitatu (3) vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kuigiza ngonjera.

i. _____

ii. _____

iii. _____

b) Eleza maana za istilahi zifuatazo za fasihi.

i. Sanaa za maonesho

ii. Taswira

c) "Fasihi simulizi ikihifadhiwa katika kanda za kunasa sauti inapoteza uhai wake." Toa hoja mbili (2) kuthibitisha kauli hii.

i. _____

ii. _____

- d) Tarihi, ngano, vigano, sogu na visasili ni vipera vya utanzu gani wa Fasihi simulizi?

- e) Eleza kwa ufupi busara za methali zifuatazo.

- i. Mtegemea cha ndugu hufa masikini.

- ii. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

SEHEMU D: (Alama 20)

UANDISHI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

9. Fafanua mambo matano (5) muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika Insha za Hoja.

AU

Chagua kichwa cha habari kimoja kati ya vifuatavyo na uandike Insha isiyopungua maneno 120 na isiyozidi maneno 150.

- UTAMADUNI WA MZANZIBARI
- MALEZI BORA KWA WATOTO

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]

10. Eleza tafauti tano (5) zilizopo kati ya barua ya kirafiki na barua ya kikazi.

This image shows a single sheet of white paper with horizontal blue ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

[illegible]

